**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

# TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA KUHUSU UTEKELEZAJI WA OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO) WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016; PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

**MEI 2016**

**YALIYOMO**

1. UTANGULIZI..................................................................................................3

2.0 UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016...........................................................................................4

3.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA OFISI YA MAKAMU WA RAIS KUHUSU UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016.................................................................................................................7

3.1 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA OFISI YA MAKAMU WA RAIS KUHUSU UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI 2015/2016.......................................................................7

3.2 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA USHAURI WA KAMATI..........................................9

4. UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017...............................................................................10

5. MAPITIO YA BAJETI OFISI YA MAKAMU WA RAIS FUNGU 26 NA 31.......................11

6.1 MAONI NA USHAURI WA KAMATI.........................................................................11

6.2 FUNGU 31...............................................................................................................12

6.3 FUNGU 26...............................................................................................................12

7. HITIMISHO...............................................................................................................13

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO) KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016; PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017**

## 1. UTANGULIZI

**Mheshimwa Spika,** napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunijalia uhai, afya njema na kunipa fursa ya kuwasilisha Taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu,

**Mheshimiwa Spika,** Waasisi wa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, Hayati Mwalimu Julius Nyerere na aliyekuwa Rais wa Zanzibar, Hayati Sheikh Abeid Amani Karume walifanikisha uundwaji wa Tanzania hapo tarehe 26 Aprili, 1964 ambapo, Sheria za Muungano zilitoa tamko la Jamhuri ya Muungano katika Ibara ya 4 kwamba:

*"Jamhuri ya Tanganyika na Jamhuri ya Watu wa Zanzibar zitalazimika, baada ya kuungana na siku zote baada ya kuungana, kuunganishwa kuwa Dola ya Jamhuri kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar' (Ibara ya 4 Sheria za Muungano)"*

Jina hili la "Jamhuri ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar" lilibadilishwa baadae mnamo tarehe 28 Oktoba, 1964 na kuwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kupitia Sheria ya Jamhuri ya Muungano, Sheria namba 61 ya mwaka 1964, ambayo ndiyo misingi ya nchi yetu. Mwaka huu, Rais wetu mzalendo, Dr. John Pombe Magufuli, ambaye ninamuona ni miongoni mwa watu wachache ambao huzaliwa katika Dunia, wenye dhamira ya dhati ya kupambana na ufisadi, kuweka maslahi ya Taifa mbele, na kusaidia kuondoa tabaka kubwa la wenye nacho na wasio nacho, alielekeza fedha za sherehe za siku husika, kusaidia ukarabati wa Barabara zetu ili kuondoa msongamano na kukuza uchumi wa nchi yetu, kwa niaba ya kamati yangu, tunampongeza kwakuwa miongoni mwa viongozi wachache wa Dunia hii wenye uwezo wa kufanya maamuzi magumu kwa maslahi ya waliowengi.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016**,** naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano

kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016; pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa kifungu 6 (2) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, Kamati ya Katiba na Sheria ina jukumu la kusimamia bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais- Muungano.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria ilifanya ziara ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa na kupokea fedha katika Mwaka wa Fedha 2015/2016 tarehe 01 Aprili 2016 katika Ofisi ya Makamu wa Rais. Kamati pia ilifanya uchambuzi wa bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano Tarehe 14 Aprili 2016. Kwa mujibu wa Kanuni ya 98 (2), Kamati pia ilichambua taarifa za utekelezaji wa bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano kwa mwaka wa fedha 2015/2016 ili kufanya ulinganisho kuhusu Makadirio ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka unaoisha na Makadirio ya Matumizi ya Fedha kwa Mwaka wa fedha 2016/2017.

**Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Makamu wa Rais ina mafungu 2 ya bajeti ambayo ni ;

i) **Fungu 31** - Ofisi ya Makamu wa Rais
ii) **Fungu 26** - Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais

**Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla taarifa hii inatoa maelezo kuhusu maeneo makubwa manne yafuatayo:-

i) Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo;
ii) Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016; na Utekelezaji wa Mapendekezo na Ushauri wa Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016;
iii) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017;
iv) Maoni na Ushauri wa Kamati.

## 2.0 UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016

**Mheshimiwa Spika,** Kanuni ya 98 (1) na 98 (2) inazitaka Kamati za Kisekta kutembelea na kukagua Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha unaoisha. Katika kutekeleza masharti ya Kanuni hiyo, Kamati ya Katiba na Sheria ilitembelea, kukagua na kupokea taarifa ya utekelezaji wa mradi Na. 6309 ulio chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais tarehe 01 Aprili 2016. Mradi huu unahusu ujenzi na ukarabati wa Ofisi ya Makamu wa Rais iliyoko barabara ya Luthuli Dar es Salaam.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati pia ilipokea taarifa ya utekelezaji wa mradi Na. 6389 unaohusu ujenzi wa Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais, Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2015/2016 Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano ilitengewa jumla ya Shilingi Bilioni Tatu, Milioni Mia Nane Sitini na Nane, Laki Nane Arobaini na Saba Elfu (3,868,847,000) kwa ajili ya Miradi mbali mbali ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, Shilingi Bilioni Mbili,Milioni Mia Nane Hamsini Elfu (2,850,000,000) ni Fedha za ndani na Shilingi Bilioni Moja,Milioni 18,Mia Nane Arobaini na Saba Elfu (1,018,847,000) ni Fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika**, mradi wa ujenzi na ukarabati wa Ofisi ya Makamu wa Rais ulitengewa Shilingi Milioni Mia Nane (800,000,000) kwenye Fungu 31 ambazo ni fedha za ndani. Mradi Na 6389 ambao ni ujenzi wa Makazi na Ofisi ya Makamu wa Rais, Tunguu, Zanzibar ulitengewa Shilingi Milioni Mia Tatu (300,000,000) ambazo hazikutolewa.

**MAONI YA JUMLA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ina maoni ya jumla yafuatayo kuhusu miradi iliyokaguliwa chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano;

- **MRADI NA. 6309 (UJENZI NA UKARABATI WA OFISI YA MAKAMU WA RAIS-LUTHULI NA IKULU NDOGO)**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati haikuridhishwa na ubora wa jengo la Ofisi ya Makamu wa Rais na mchanganuo wa matumizi ya fedha za mradi kama ulivyowasilishwa mbele ya Kamati. Kutokana na kutoridhishwa na hali hii Kamati ilitoa maagizo yafuatayo;

i) Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (Controller and Auditor General- CAG) kufanya ukaguzi na uchunguzi wa kina wa thamani ya jengo na fedha zilizotumika katika mradi huu (Value for Money) na taarifa ya uchunguzi huu iwasilishwe mbele ya Kamati ili kuiwezesha kutoa ushauri sahihi .

ii) Hatua kali za kisheria na kinidhamu zichukuliwe kwa Watumishi/Watendaji wote waliohusika na mradi huu kwa mujibu wa sheria endapo itathibitika kwamba wamehusika katika matumizi mabaya ya fedha za Serikali na hatua hizi za kisheria ziwe za kijinai au za kimadai.

iii) Malipo yote yaliyobaki ya wakandarasi katika mradi huu yasitishwe mpaka uchunguzi kamili utakapokamilika na wakandarasi wote waliohusika na mradi kuwajibika endapo itathibitika kwamba jengo hili limejengwa chini ya kiwango.

iv) Vilevile kwa tahadhari ya usalama Kamati ilishauri Ofisi ya Makamu wa Rais kuondoa milango yote ya vioo ya kuzunguka (Round) katika jengo ambayo inahatarisha usalama wa watumiaji endapo kutatokea janga la moto au hatari yoyote inayohitaji msaada wa haraka.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilikutana tena na Waziri wa Nchi- Ofisi ya Makamu wa Rais, Naibu Waziri pamoja na Watendaji Wakuu wa Ofisi ya Makamu wa Rais tarehe 14 Aprili 2016 wakati wa uchambuzi wa taarifa ya bajeti za Ofisi ya Makamu wa Rais na kusisitiza tena kuhusu utekelezaji wa Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kuhusu mradi huu.Aidha Kamati inasubiri taarifa ya Mkaguzi wa Hesabu za Serikali na taarifa kutoka Kitengo cha Hazina cha Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo ya Serikali ili iweze kutoa maoni na ushauri kuhusu suala hili.

- **MRADI NA. 6389 - UJENZI WA OFISI NA MAKAZI YA MAKAMU WA RAIS, ZANZIBAR**

**Mheshimiwa Spika**, kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 mradi huu ulitengewa Shilingi Bilioni Mia Tatu (300,000,000).Hata hivyo Kamati iliarifiwa kwamba fedha hizo hazikutolewa. Kamati ilishauri Ofisi ya Makamu wa Rais kuwa mara ipatapo fedha ujenzi wa Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais ukamilishwe kwa haraka.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatoa rai kwa Serikali kuongeza fedha zinazotengwa katika miradi ya maendeleo ya Muungano ili kuendelea kupunguza kero za Muungano na kuudumisha Muungano wa Tanganyika na Zanzibar uliodumu kwa muda wa miaka 52 sasa.

## 3.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA OFISI YA MAKAMU WA RAIS KUHUSU UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016

### 3.1 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA OFISI YA MAKAMU WA RAIS KUHUSU UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI 2015/2016

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 98 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016 Kamati ilikutana Jijini Dar es Saalam tarehe 14 Aprili, 2016 kwa ajili ya uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 na uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017. Kamati ilipata fursa ya kuchambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti za mafungu yote mawili yaliyo chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano.

**Mheshimiwa Spika,** katika uchambuzi wa utekelezaji Mpango wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais -Muungano kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 Kamati ilizingatia mlinganisho wa kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge Mei 2015 na kiwango ambacho kimepokelewa hadi Machi 2016.

**Mheshimiwa Spika**, Lengo la kufanya tathmini ya namna hii ni kufahamu Mwelekeo wa Mpango wa Bajeti ya Mapato na Matumizi ya Serikali katika Mwaka wa Fedha 2015/2016 ili kujua vipaumbele vya kibajeti katika Mwaka wa Fedha ujao. Hata hivyo uchambuzi huu haukuhusisha kifungu 5001 kinachohusika na masuala ya Mazingira kwani Kamati ya Katiba na Sheria haihusiki nacho. Aidha, uchambuzi haukuhusu suala la ukusanyaji wa maduhuli kwani Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano haina vyanzo vyovyote vya mapato.

### i) OFISI BINAFSI YA MAKAMU WA RAIS (FUNGU 26)

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2015/2016 Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais, Fungu 26, ilidhiinishiwa Shilingi Bilioni Tatu, Milioni Mia Sita Hamsini na Saba, Mia Tano na Themanini na Nne Elfu (3,657,584,000). Kati ya fedha hizo, Shilingi Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Nne Themanini, Mia Sita Sabini na Sita Elfu (1,480,676,000) ni kwa ajili ya Mishahara na Shilingi Bilioni Mbili, Milioni Mia Moja Sabini na Sita, Mia Tisa na Nane Elfu (2,176,908,000/=) ni za Matumizi Mengineyo

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2016 Fungu 26 lilipokea kiasi cha Shilingi Bilioni Mbili, Milioni Mia Mbili na Ishirini, Mia Nane Kumi na Nne Elfu, Mia Sita Arobaini na Tatu (2,220,814,643/ ) sawa na asilimia 60.7 ya bajeti yote. Kati ya fedha

zilizopokelewa, Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Nne Sitini na Tano, Mia Nne Sabini na Tatu Elfu, Mia Sita Arobaini na Tatu (1,465,473,643) ni za Matumizi Mengineyo, sawa asilimia 67.3 ya Bajeti ya Matumizi Mengineyo, na Shilingi Milioni Mia Saba Hamsini na Tano, Laki Tatu Arobaini na Moja Elfu (755,341,000) ni za Mishahara, sawa na asilimia 51 ya Bajeti ya Mishahara.

**Jedwali Na.01: Mchanganuo wa Fedha Zilizoidhinishwa na Kupokelewa Chini ya Fungu 26 katika Mwaka wa Fedha 2015/2016**

| | **Fedha Zilizoidhinishwa** | **Fedha Zilizopokelewa** | **Asilimia** |
|---|---|---|---|
| Kawaida | Sh. 2,176,908,000 | Sh. 1,465,473,643 | 67.3 |
| Mishahara | Sh. 1,480,676,000 | Sh. 755,341,000 | 51 |
| Maendeleo | 0 | 0 | 0 |
| Jumla | 3,657,584,000 | 2,220,814,643 | 118.3 |

### ii) OFISI YA MAKAMU WA RAIS (FUNGU 31)

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2015/2016 Ofisi ya Makamu wa Rais, Fungu 31, iliidhinishiwa jumla ya Shilingi Bilioni Thelathini na Tano, Milioni Mia Tatu Thelathini na Tano, Mia Saba Hamsini na Nne Elfu (35,335,754,000). Kati ya fedha hizo Shilingi Bilioni Thelathini na Moja, Milioni Mia Nne Sitini na Sita, Mia Tisa na Saba Elfu (31,466,907,000) ni fedha za Matumizi ya Kawaida na Shilingi Bilioni Tatu, Milioni Mia Nane Sitini na Nane, Mia Nane Arobaini na Saba Elfu (3,868,847,000) ni fedha za Miradi ya Maendeleo.

Hadi kufikia Machi 2016, Ofisi ilipokea Shilingi Bilioni Thelathini na Tatu, Milioni Mia Tano Themanini na Tisa, Mia Sita Arobaini na Saba Elfu na Thelathini na Tano (33,589,647,035). Kati ya Fedha hizo Shilingi Bilioni Ishirini na Saba, Milioni Mia Tano Tisini na Tano, Mia Tisa Sitini na Tatu Elfu (27,595,963,000) ni gawio kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

**Jedwali Na.02: Mchanganuo wa Fedha Zilizoidhinishwa na Kupokelewa Chini ya Fungu 31 katika Mwaka wa Fedha 2015/2016**

| | Fedha Zilizoidhinishwa | Fedha Zilizopokelewa | Asilimia |
|---|---|---|---|
| Kawaida | Sh. 31,466,907,000 | Sh. 1,685,522.961 | 5.5 |
| Mishahara | Sh. 1,480,676,000 | Sh. 2,180,848,003 | 147.3 |
| Maendeleo | Sh. 3,868,847,000 | Sh. 338,079,000 | 8.7 |
| Jumla | Sh. 36,816,430,000 | Sh. 4,204,449,964 | 11 |

### 3.2 Mapitio ya Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati

**Mheshimiwa Spika**, Kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016, Kamati ilitoa mapendekezo matano kuhusiana na Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba yapo maagizo yameshatekelezwa na mengine ambayo yanaendelea kutekelezwa na Ofisi ya Makamu wa Rais.

**Mheshimiwa Spika**, maoni ambayo hayakutekelezwa kikamilifu mpaka sasa ni kama ifuatavyo:

i) Serikali kutenga Bajeti ya kutosha na kutoa fedha zinazoidhinishwa na Bunge kwa wakati;

ii) Serikali kutenga fedha kwa ajili ya kununua magari mapya ili kuepuka gharama za matengenezo ya mara kwa mara ya magari yaliyochakaa;

iii) Maadhimisho ya Sherehe za Muungano yahamasishwe na kufanyika katika ngazi za Wilaya na Mikoa ili kuwawezesha Wananchi wengi kupata elimu sahihi ya Muungano.

**Mheshimiwa Spika**, Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais imeendelea kuwa ndogo hivyo kuathiri ufanisi katika kutekeleza majukumu yake kama inavyoonyesha kwenye jedwali hapa chini.

**Jedwali Na.03: Tofauti ya Kiasi cha Fedha Kilichoidhinishwa 2015/2016 na Kinachoombwa 2016/2017 Katika Mafungu 31 na 26.**

| Fungu | Fedha Iliyoidhinishwa | Maombi Ya Fedha Mwaka | Tofauti | Asilimia |
|---|---|---|---|---|

| | **2015/2016** | **2016/2017** | | |
|---|---|---|---|---|
| 26 | Sh. 3,657,584,000 | Sh. 3,646,184,000 | Sh.11,400,000 | 0.3 |
| 31 | Sh.35,335,754,000 | Sh.20,386,699,448 | Sh.14,949,054,552 | 57.1 |

## 4. UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

**Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano imepanga kutekeleza lengo moja (1) tu la Uratibu wa Masuala ya Muungano kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017. Katika kuhakikisha lengo hili linafanikiwa Ofisi imejipanga kutekeleza shughuli zifuatazo:

i) Kuratibu vikao viwili (2) vya Kamati ya Pamoja ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Vikao hivyo vitatanguliwa na vikao viwili (2) vya Mawaziri na Makatibu Wakuu kutoka pande zote mbili za Muungano na vikao vitano (5) vya Sekretarieti ya Kamati ya Pamoja ya Serikali za pande zote mbili za Muungano; Vikao vya aina hii viliratibiwa na Serikali ya awamu iliyopita, ambapo vikao tisa (9) vilifanyika kwa nyakati na maeneo tofauti chini ya Uenyekiti wa Makamu wa Rais ili kujadili na kutatua changamoto za Muungano.Kati ya mwaka 2006 hadi 2011 jumla ya hoja kumi na tano (15) ziliwasilishwa na kujadiliwa na kamati ya pamoja ya (SMT) na (SMZ). Kati ya hizo hoja kumi na mbili (12) zimepatiwa ufumbuzi na hoja tatu (3) zipo katika hatua mbalimbali za kupatiwa ufumbuzi.

ii) Kuelimisha Umma kuhusu Muungano;

iii) Kuratibu utekelezaji wa masuala ya kiuchumi na kijamii kwa faida ya pande zote mbili za Muungano;

iv) Kuratibu ushirikiano wa Wizara na Taasisi zisizo za Muungano zenye majukumu yanayoshabihiana kutoka pande zote mbili kukutana mara mbili (2) kwa mwaka kwa ajili ya kuimarisha masuala yasiyo ya Muungano.

## 5. MAPITIO YA BAJETI OFISI YA MAKAMU WA RAIS-MUUNGANO FUNGU 26 NA 31 KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

### OFISI BINAFSI YA MAKAMU WA RAIS-FUNGU 26

**Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais, (Fungu 26) inaomba kuidhinishiwa Shilingi Bilioni Tatu, Milioni Mia Sita Arobaini na Sita, Mia Moja Themanini na Nne Elfu (3,646,184,000). Kati ya Fedha hizo Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Moja na Arobaini na Sita, Mia Tatu Themanini na Nne Elfu (1,146,384,000) ni kwa ajili ya Mishahara na Shilingi Bilioni Mbili, Milioni Mia Nne Tisini na Tisa na Mia Nane Elfu (2,499,800,000) ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Katika maombi ya Mwaka wa Fedha 2016/2017 kumekuwa na punguzo la Shilingi Milioni Kumi na Moja, Laki Nne (11,400,000) ukilinganisha na Fedha iliyoidhinishwa katika Mwaka wa Fedha 2015/2016. Kiasi hiki ni asilimia 0.3 %

**OFISI YA MAKAMU WA RAIS FUNGU 31**

**Mheshimiwa Spika,**kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano (Fungu 31) inaomba kuidhinishiwa jumla ya Shilingi Bilioni Kumi na Saba, Milioni Mia Saba Arobaini na Saba Ishirini na Tano Elfu (17,747,025,000). Kati ya Fedha hizo Shilingi Bilioni Sita, Milioni Mia Nane Sabini na Tisa, Mia Saba Sabini na Tano Elfu (6,879,775,000) ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi Bilioni Kumi, Milioni Mia Saba Arobaini na Saba, Mia Mbili na Hamsini Elfu (10,747,250,000) ni Fedha za Miradi ya Maendeleo. Katika Maombi ya Mwaka wa Fedha 2016/2017 kumekuwa na punguzo kubwa la fedha kiasi cha Shilingi Bilioni Kumi na Saba, Milioni Mia Saba na Nane, Mia Saba Ishirini na Tisa Elfu (17,708,729,000) ikilinganishwa na fedha zilizoidhinishwa katika Mwaka wa Fedha 2015/2016. Punguzo hilo ni nusu ya fedha iliyoombwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 sawa na asilimia 50.2%

**Mheshimiwa Spika**, punguzo hili la fedha litaathiri utekelezaji wa majukumu ya Ofisi hii hivyo kuna haja ya Serikali kufikiria upya suala la ukomo wa bajeti ili kuwezesha Taasisi zake kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

## 6.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, naomba sasa kutoa maoni na ushauri wa Kamati kuhusu masuala yaliyobainika wakati wa uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais Fungu 31 na Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais Fungu 26 kama ifuatavyo:

### 6.1 FUNGU 31-OFISI YA MAKAMU WA RAIS

i) Kutokana na Serikali kujenga Jengo la Ofisi ya Makamu wa Rais Dar es Salaam chini ya kiwango, Kamati inashauri Serikali kuwa makini wakati wa uteuzi wa Wakandarasi ili kuhakikisha kuwa wanaopewa tenda za ujenzi wa Ofisi nyeti kama ya Makamu wa Rais wanakuwa na uadilifu, uwezo, ujuzi na weledi wa hali ya juu. Aidha, Wakala wa Majengo ya Serikali (Tanzania Building Agency-TBA)

uwe makini wakati wote kukagua na kuhakikisha kuwa majengo ya Serikali yanajengwa kwa ubora na kwa viwango stahiki. Pia Wakala huo uhakikishe kwamba Serikali kwa namna yoyote ile haikabidhiwi jengo lililojengwa chini ya kiwango kuepusha kupata hasara.

ii) Serikali itenge Bajeti ya kutosha na kutoa fedha zinazoidhinishwa kwa wakati hasa kwenye Miradi ya Maendeleo kwani imebainika kuwa fedha zilizopokelewa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo katika Mwaka wa Fedha 2015/2016 ni kiasi kidogo sana ukilinganisha na fedha iliyoombwa na kuidhinishwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi yote iliyoko kwenye Fungu 31. Pia ipo miradi ambayo haikupokea fedha kabisa.

iii) Serikali iendelee kutoa elimu kwa Wananchi kuhusu umuhimu na faida zinazotokana na Muungano wa Pande zote mbili ili Wananchi waone ulazima wa kuuthamini, kuupenda, kuudumisha na kuulinda Muungano huu kwa maslahi ya nchi yetu, kizazi cha sasa na vizazi vijavyo.

iv) Serikali iendelee kuchukua jitihada za dhati katika kutatua kero za Muungano ili kuongeza tija katika shughuli mbalimbali za biashara na maendeleo kati ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar.

### 6.2 FUNGU 26-OFISI BINAFSI YA MAKAMU WA RAIS

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inashauri Ofisi Binafsi ya Makamu wa Raisi iendelee kuwezeshwa kifedha ili Mheshimiwa Makamu wa Rais aweze kutimiza majukumu yake kwa ufanisi

## 7. HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, mwisho napenda kukushukuru wewe binafsi, Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi hii muhimu kuwasilisha maoni ya Kamati. Aidha, sina budi kukupongeza wewe binafsi, Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa kuliongoza Bunge letu Tukufu kwa busara, umakini na umahiri mkubwa.

**Mheshimiwa Spika**, napenda nitumie nafasi hii pia kumshukuru Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano, Mheshimiwa January Yusuph Makamba, Mb, Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, Mb, Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais Mheshimiwa Mbarak Mohammed Abdulwakil ,Naibu Katibu Mkuu,Ofisi ya Makamu wa Rais Mhandisi Ngosi Charlestino Mwihava na Watendaji wote wa Ofisi ya Makamu wa Rais- Muungano kwa ushirikiano mkubwa

walioutoa kwa Kamati wakati wa uchambuzi wa Makadirio na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano.

**Mheshimiwa Spika**, kipekee niwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa kazi nzuri ya kujadili na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017. Uzalendo na uchapakazi wao pamoja na ushirikiano mkubwa waliotoa umesaidia kufanikisha kukamilika kwa Taarifa hii kwa wakati. Kwa ruhusa yako naomba niwatambue Wajumbe wa Kamati kama ifuatavyo:

(i) Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa, Mb- Mwenyekiti

(ii) Mhe. Najma Mutraza Giga, Mb- Makamu Mwenyekiti

(iii) Mhe. Selemani Jumanne Zedi, Mb,Mjumbe

(iv) Mhe. Ally Saleh Ally, Mb, Mjumbe

(v) Mhe. Mboni Mohamed Mhita, Mb, Mjumbe

(vi) Mhe. Taska Restituta Mbogo, Mb, Mjumbe

(vii) Mhe. Makame Mashaka Foum, Mb, Mjumbe

(viii) Mhe. Seif Ungando Ally, Mb, Mjumbe

(ix) Mhe. Richard Mganga Ndassa, Mb, Mjumbe

(x) Mhe. Nassor Suleiman Omar, Mb, Mjumbe

(xi) Mhe. Saumu Heri Sakala, Mb, Mjumbe

(xii) Mhe. Twahir Awesu Mohamed, Mb, Mjumbe

(xiii) Mhe. Dkt. Godwin Aloyce Mollel, Mb, Mjumbe

(xiv) Mhe. Asha Abdallah Juma, Mb, Mjumbe

(xv) Mhe. Ajali Rashid Akbar, Mb, Mjumbe

(xvi) Mhe. Omary Ahmed Badwel, Mb, Mjumbe

(xvii) Mhe. Joseph Kizito Mhagama, Mb, Mjumbe

(xviii) Mhe. Riziki Shahari Mngwali, Mb, Mjumbe

(xix) Mhe. Joram Ismael Hongoli, Mb, Mjumbe

(xx) Mhe. Anna Joram Gidarya, Mb, Mjumbe

(xxi) Mhe. Gibson Blasius Meiseyeki, Mb, Mjumbe

(xxii) Mhe. Rashid Abdallah Shangazi, Mb, Mjumbe

(xxiii) Mhe.Mathayo David Mathayo, Mb, Mjumbe

(xxiv) Mhe. Suleiman Masoud Nchambi, Mb, Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuwashukuru kwa dhati Watumishi wa Ofisi ya Bunge, chini ya Uongozi wa Dkt Thomas D. Kashillah, Katibu wa Bunge, kwa kusaidia na kuiwezesha Kamati kutekeleza Majukumu yake. Kipekee , nawashukuru Ndugu Angelina Sanga, Stella Bwimbo, Stanslous Kagisa, Dunford Mpelumbe na Gaitana Chima kwa kuratibu vyema kazi za Kamati na kuhakikisha kuwa Taarifa hii inakamilika kwa wakati uliopangwa.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo, sasa naomba Bunge lako Tukufu, likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais- Muungano (Fungu 31) na Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais(Fungu 26) kama yalivyowasilishwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na naunga mkono Hoja.

Mohamed Omary Mchengerwa, Mb.

**MWENYEKITI,**

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA**

**02 Mei, 2016**